HALMASHAURI YA MJI MAFINGA

SHULE YA SEKONDARI LUGANGA
S.L.P 454
MAFINGA
11/12/2020

Kumb Na. **HM/MAF/LGG/SS/JIF/2021**
Jina la Mwanafunzi……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUGANGA MJI WA MAFINGA MKOA WA IRINGA MWAKA 2021

A. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya Sekondari Luganga ipo umbali wa kilometa tano (5) kaskazini/mashariki mwa Mji wa Mafinga. Usafiri kutoka kituo cha mabasi stendi ni wa bajaji au bodaboda, ikiwa bajaji ni shilingi miatano(500) na bodaboda ni shilingi elfumbili (2000).

Mhulawa kwanza wa masomo unaanza Tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **22/01/2021**.

B.MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

i. Sare za Shule

a). Sare ya shule hii ni zambarau kwa wa sichana na shati jeupe mikono mirefu aina ya tomato.

Kwa wasichana (sketi 2 na shati 2). Maelekezo ya mshono ni Linda Box iwe ndefu mpaka miguuni.

b).Tai kwa wasichana ifanane na rangi ya sketi.

c). Sare ya wavulana ni rangi ya udongo na shati la tomato (suruali 2 nashati 2)

d).Tai kwa wavulana ifanane na rangi ya suruali.

e). Rangi ya hijabu nyeupe

f). Sare za michezo kwa shule hii upande wa wa vulana na wa sichana ni
(raba nyeusi, na tracksuit darckblue)

g). Wavulana na wasichana (sweta rangi ya darkblue)

h). Viatu vya shule ni rangi nyeusi vya ngozi view na kamba, visiwena kisigino kirefu.

i). Pullneck nyeusi kwaajili ya kuvalia na shati

ii. Kila mwanafunzi lazima awe na cheti cha kuzaliwa kinapatikana Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Mafinga (Bomani). Ujena kopi yake.

iii. Daftari 9 za masomo (kaunta) na daftari msomi 9 kwa ajili ya mazoezi ya kila siku, kalamu, na mkebe kwa ajili ya hesabu.

iv.Chakula cha wanafunzi wakutwa kitatakiwa kiwepo mwaka mzima kwamichango toka kwa mzazi wa mtoto husika, utaratibu utafanyika jinsi ya kuchangia chakula na kamati ya wazazi mara baada ya mtoto kujiunga na Shule.

3.0 Sheria na kanuni muhimu za shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa (OR-TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

3.1 Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara utakapokuwa umeripoti shuleni

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lzima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za shule na za umma popote zilipo.

3.2 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, kama vile uvutaji bangi,Cocaine, Mirungi, Kubeli na Kadhalika.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali za umma.
7. Kudharau Bendera ya Taifa.
8. Kuwa na mimba au kusababisha mimba.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kutoa mimba.

11. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa au kugoma adhabu kwa makusudi
13. Kuwa na simu ya mkonini
14. Utoro sugu

4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopaswa kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi:

1) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali .Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni.
2) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kuto shiriki migomo, fujo, na makosa ya jinai.
3) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelezo mengine ya takayo tolewa na Shule.

5.0 Tafadhali soma kwa makini maelezo /maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA SHULENI LUGANGA SEKONDARI

…….

WILLIAM CHOTTA UVAMBE

MKUU WA SHULE

FOMU YA AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi……Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi…….aliye chaguliwa kujiunga katika Shule ya Sekondari Luganga. Ninakubali Mwangu asome katika shule hii kwa kufuata kanuni na taratibu za shule kama zilivyo ainishwa kwenye miongozo ya Elimu.

Saini ya Mzazi/Mlezi……

Tarehe……..

FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi …….mwanafunzi wa Shule ya Sekonsdari Luganga. Ninakubali kujiunga na Shule hii kwa kufuata kanuni na taratibu za shule, ikiwa ni pamoja na kuwa na nidhamu nzuri, kuwa mtiifu, mahudhurio mazuri shuleni n.k

Saini ya Mwanafunzi……

Tarehe……...

SHULE YA SEKONDARI LUGANGA
S.L.P 454- MAFINGA

FOMU YA KUPOKELEWA SHULENI

1. Jina kamili……...……Jinsia KE/ME
2. Mahali alipozaliwa, Mkoa……..Wilaya……..Kata……..
3. Tarehe ya kuzaliwa……....
4. Uraia……..
5. Anuani ya Mzazi/Mlezi…….
6. Jina la Mzazi/Mlezi……
7. Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi……
8. Dini ……...
9. Kidato alichopokelewa……..
10. Shule aliyotoka……..
11. Michezo anayopendelea…….
12. Namba ya mitihani TSM9……..
13. Kazi/Shughuli ya Mzazi/Mlezi……..

SHULE YA SEKONDARI LUGANGA
S.L.P 454- MAFINGA

DAKTARI

HOSPITALI YA……

S.L.P……...

FOMU YA UPIMAJI WA AFYA YA MWANAFUNZI

Tafadhali husika na kichwa tajwa,

Unaombwa kupima mwanafunzi aitwaye……

Wakidato cha kwanza Mwaka 2020/2021

Ili kufahamu afya yake kama anaweza kuhudhuria masomo katika shule hii.

…….

WILLIAM CHOTTA UVAMBE
MKUU WA SHULE

IJAZWE NA DAKTARI

VIPIMO

HB:……	FBP:……
UPT:…….	VDRL…….
Widal Test:……	Urinalysis:……..
Tube(Blood Group):…….	Stool Analysis:……...

Mimi Dr……..wa Hospitali ya……..iliyopo…….

Nimempima mwanafunzi mtajwa hapo juu na kugundua anayo/hana matatizo. Maoni na mapendekezo ya daktari.

……
……

…….
Saini na Muhuri